



Kusanidi Tableti Yako Uliyopewa na RPS


① Ikiwa tableti yako imezimwa, bonyeza na ushikilie kitufe cha nishati upande wa kulia wa kifaa.



② Chagua lugha inayofaa kisha ubofye kishale ili kuendelea.




③ Kubali **Terms and Conditions** zote kwa kuweka tiki vipengele vyote na kisha. Kisha bofya **Next**.




④ Kutoka kwenye skrini ya **Wi-Fi**, chagua mtandao kisha weka nenosiri.




⑤ Chagua **Don't copy** kutoka kwenye skrini ya **Copy apps & data** ili uendelee.




⑥ Ingia kwa kutumia **RPS account and password** kwenye skrini inayofuata. Hii itahifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya baadaye.



⑦ Kutoka kwenye skrini ya Huduma za Google, washa au zima uteuzi wowote kisha bofya Kubali.




⑧ Unaweza kulinda tableti kwa kutumia pin au nenosiri. **Tafadhali kumbuka: RPS haiwezi kuweka upya chaguo hili.**




Kusanidi Tableti Yako Uliyopewa na RPS


⑨ Chagua **Skip** kutoka kwenye skrini ya Ingia kwenye akaunti yako ya Samsung.




⑩ Usanidi unapokamilika, utaarifiwa. **Bofya Finish** ili ufikie programu za tableti.



Google Classroom inapatikana kutoka kwenye skrini yako ya mwanzo. Chagua akaunti yako ya RPS kutoka kwenye orodha ili ufikie madarasa yako.



Skrini ya Mwanzo ya Tableti Yako



Google Meet inapatikana pia kutoka kwenye skrini yako ya Mwanzo. Hii itakuwezesha kuwasiliana na mwalimu wako wakati wa vikao vya darasa vya mtandaoni.

Ukikosa kuona programu kutoka kwenye skrini yako ya mwanzo, telezesha juu kuanzia chini ili uone orodha kamili inayopatikana.